**OFISI YA RAISI (TAMISEMI)**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA**

SHULE YA SEKONDARI MAGADINI,
S. L P 41,
SANYA JUU, SIHA.
30/05/2021

MZAZI/ MLEZI WA ……………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAGADINI.**

Jumuiya ya shule ya sekondari Magadini inayofuraha ya kukujulisha kuwa mwanao …………………………………………………………… amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika mwaka wa masomo 2021/2022. Hongera sana. Shule ya sekondari Magadini iliyopo wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, kanda ya Kaskasini itafunguliwa tarehe ……………………………….. Mwanafunzi anatakiwa kuripoti kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi na moja kamili jioni na mahitaji yote yaliyoainishwa.

## 1. MAHALI SHULE ILIPO

Basi unalosafiri nalo ikifika standi kuu ya Moshi mjini, Upande magari yanayoelekea standi ya Sanya juu kwa nauli ya shilingi Tsh. 2000/=. Ukitokea Arusha hadi Bomang'ombe unaweza kupanda gari la kuelekea Sanya juu standi kwa shilingi 1,000. Kisha usafiri wa kuelekea shule ya sekondari magadini ni shilingi 7,000/= kwa Taxi au shilingi 3000/= kwa pikipiki,kwa bajaji 5000.

## 2. MALIPO YA MAHITAJI YA SHULE

### 2.1 ADA NA MALIPO MENGINE

| **Mahitaji** | **Kiasi cha fedha (tsh.)** | **Maelezo yake** | **Weaka kwenyeAkaunti namba** |
|---|---|---|---|
| Ada | 70,000 | Kwa mwaka mzima | 4011200098 |
| Tahadhari | 5,000 | Mara moja na hairudishwi | 4012300381 |
| Mpishi | 10,000 | Kwa mwaka mzima | 4012300381 |
| Mlinzi | 10,000 | Kwa mwaka mzima | 4012300381 |
| Picha na kitambulisho | 5,000 | Mara moja | 4012300381 |
| Matron | 10, 000 | Kwa mwaka mzima | 4012300381 |
| Ukarabati na madawati | 15,000 | Mara moja | 4012300381 |
| Taaluma | 20,000 | Kwa mwaka mzima | 4012300381 |
| Matibabu | 15,000 | Kwa mwaka mzima | 4012300381 |
| **Jumla** | **160,000** | | |

### 2.2 SARE ZA SHULE NA MAHITAJI MENGINE

Mwanafunzi anapokuja shuleni aje na vifaa vifuatavyo:

- Sanduku imara la chuma na kufuli,
- Blanketi moja nzito,
- Viatu vyeusi vyenye kisigino kifupi vyenye kamba**,**
- Mashuka mawili ya rangi ya pinki,
- Mto na Faronya ya rangi ya pinki,
- Neti ya kujikinga na mmbu.

- Soksi nyeupe ndefu jozi mbili.
- Sketi rangi ya bluu ya michezo, T. shirt nyeupe na raba ya michezo,
- Track suit nzito yenye rangi nyeusi na mistari nyeupe pembeni (zisiwe za kubana)
- Ndoo ndogo moja,
- Mabuti kwa ajili ya matope wakati wa mvua,
- Tochi ya betri,
- Scientific calculator
- Sahani, kijiko na vikombe vya bati.
- Mwanafunzi wa HGK aje na hard broom, jembe na mpini.
- Mwanafunzi wa HGL aje na brush za chooni, slasher na moper.
- Vitabu vya tahasusi atakayosoma mwanafunzi.
- Rimu 1 (A4) plain kwa mwaka.
- Madaftari saba counter books Q2 na daftari ndogo saba za mazoezi.
- Paspoti zise moja ya rangi.

Sare(uniform) ya mwanafunzi atakayotakiwa kuja nayo ni kama ifuatavyo

| | Jina la kifaa |
|---|---|
| 1 | Sweta moja (kijani liliyo kolea) |
| 2 | Sketi mbili za sare (kijani liliyo kolea.kijani ya jeshi).rinda box, urefu 16 cmchini ya goti |
| 3 | Shati mbili nyeupe mikono mrefu |
| 4 | Gauni mbili za kushindia shuleni (Rangi damu ya mzee) mshono wa solo lifike chini ya goti cm 16 |
| 5 | Tai moja ( kijani iliyokolea yenye mistari midogo myeupe) |
| 6 | Kukodisha godoro kwa mwaka mmoja TSH 15000/= au mwanafunzi anaweza kuja na godoro lake. |

**3. MALIPO**

Ada ilipwe kwenye akaunti ya **NMB 4011200098, Magadini sekondari**.
Michango mengine ilipwe kwenye akaunti ya **NMB 4012300381, Magadini sekondari**. Mwanafunzi anapokuja shuleni aje na **pay- in slip** kwa uthibitisho. Hakuna fedha itakayopokelewa shuleni. Jitahidi kufanya malipo yako kwa wakati.

**4. MATIBABU**

Wanafunzi wenye bima waje na bima zao. Wanafunzi wasio na bima ya afya watapatiwa kitambulisho cha bima ya afya (CHF) kitakachotumika kwa mwaka moja tu. Taarifa za tatizo la afya zitolewe mapema na mwanafunzi kwa matron kwa ajili ya utaratibu wa matibabu. Endapo mwanafunzi amelazwa hospitalini atarudi mara tu atakaporuhusiwa na daktari na kuripoti kwa matron. Matibabu makubwa yatagaramikiwa na mzazi au mlezi.

**5. VIFAA VYA USAFI BINAFSI**

Mwanafunzi aje na sabuni, taulo, kandambili, rangi ya viatu vyeusi, mswaki, dawa ya mswaki, mafuta ya kupaka na nguo za ndani za kutosha. Mafuta ya kupaka aina ya **cream** na **marashi** haviruhusiwi**.**

**6. MWENENDO NA TABIA**

- Kila mwanafunzi anawajibu wa kuonyesha kiwango cha juu cha nidhamu katika kila shughuli kama vile kuwahi, ukakamavu, usafi, uaaminifu, michezo na kila jambo linalomhusu.
- Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu na kuwatii walimu, wafanyakazi wasio walimu, Wageni na walezi wengine shuleni na nje ya shule.
- Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu viranja wa shule walioteuliwa na kuchaguliwa, wanafunzi wanzake ndani na nje ya shule.

**7. NJE NA NDANI YA MIPAKA SHULE**

- Hairuhusiwi kwenda myumba na walimu na watumishi wasio walimu bila ruhusa au sababu za msingi.
- Hairuhusiwi kuingia baa, vilabu vya pombe na nyumba za kulala wageni
- Hairuhusiwi mwanafunzi kulala au kutoka nje ya shule bila kibali cha mkuu wa shule wakati wowote

**8. MAMBO YALIYOPIGWA MARUFUKU SHULENI**

- Kuonesha tabia mbaya kama vile kupigana, kupiga kelele ovyo, kutukana na ulevi wa aina yeyote
- Kukashifu dini yeyote au kabila la mtu
- Kushabikia chama chochote cha siasa
- Kuhamasisha migomo au vurugu ya aina yeyote
- Kukaribisha wageni pasipo idhini ya shule
- Kumkaribisha mgeni au mwanafunzi yeyote asiyehusika bwenini
- Kuharibu mali ya shule, umma au ya mwenzako kwa makusudi
- Kuweka dawa au kusuka nywele, kufuga kucha au kuweka rangi
- Kuvaa nguo zisizoidhinishwa kwa matumizi hapa shuleni
- Kumiliki simu ya mkononi, line ya simu au simu yeyote bila idhini ya mkuu wa shule au matron
- Kuchelewa kuripoti shuleni baada ya likizo.
- Ni marufuku mwanafunzi kufika shuleni na simu

**9. BAADHI YA MAKOSA YANAYOMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULENI**

1) Wizi
2) Uasherati, na kupata mimba
3) Kutumia kilevi cha aina yeyote
4) Makosa ya jinai
5) Kupiga au kupigana
6) Kuharibu makusudi mali ya umma
7) Kudharau bendera ya taifa, picha ya raisi au mwenge wa uhuru
8) Kuolewa
9) Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo
10) Kumiliki simu au line ya simu shuleni
11) Lugha ya matusi
12) Kugoma na kukataa adhabu
13) Kutoroka au kuondoka shuleni bila ruhusa ya mkuu wa shule.

**10. MAWASILIANO**

Mawasiliano yote yafanyike kwa namba za simu zifuatazo:

- Namba ya simu ya mkuu wa shule: **0759359466/ 0710849167**
- Namba ya simu ya makamu mkuu wa shule: **0758206826**
- Namba ya simu ya matron wa shule: **0787-667262**

Mwanafunzi anapaswa kujaza fomu ya matibabu na taarifa binafsi. Ninakutakia safari njema ya kufika hapa shule ya sekondari magadini. Karibu sana.

……………

Felista Z Kileo

Mkuu wa shule

**THE PRESDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**SIHA DISTRICT COUNCIL**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be
Completed by a medical officer in respect of all form one and five students who join secondary school

## PART A
## TO THE MEDICAL OFFICER

**……………………………………………………………………………………………………………………**
**STUDENT FULL NAME ………………………………………………………………………………………….**

Please examine the above named person as to be admitted to secondary school education
Signature ……………………………………….. Designation……………………………………………
Name of head of school……………………………………………Official stamp …………………………………………….

## PART B: TO BE COMPLETED BY MEDICAL OFFICER

Blood count (white and red) ……………………………………………………………………………..
Stool examination ………………………… TB Test ……………………………………………………….
Eye test …………………………………………… Ears test……………………………………………………………
Chest test………………………………………. Spleen test ……………………………………………………..
Abdnomen test ………………………………… pregnancy (girls only) ………………………………………

## ADDITIONAL INFORMATION

Physical defect or impairment
………………………………………………………………………………………………………….
………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………….
Infection, chronic disease or family disease
……………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
Other information
……………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………………
Please certify that the above is fit to be enrolled at Magadini secondary school
Signature …………………………… Designation ………………………………….station ……………………….
Date ………………………………

**PART C: MEDICAL OFFICER CERTIFICATION**

I have examined the above person and consider that she/ he is/not fit physically to join to secondary school.

Medical officer's name ………………………………………………………. Signature ……………………………

Date …………………………………………………………………

………………………………………………………………..
Official stamp

**HALMASHAURI YA WILAYA SIHA**

**SHULE YA SEKONDARI MAGADINI**

**TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI**

Mimi mwanafunzi …………………………………………......mwenye umri wa miaka…………

Jina kamili la baba……………………………………………………………………………….

Umri wa baba ni miaka………………Wilaya…………………… Tarafa………………..............

Kata…………………………… Namba ya simu ………………………...Dini…………………

Dhehebula…………..S.L.P………

Mimi mwanafunzi ……………………………………………………… ninakiri kukubaliana na kufuata sheria zote za shule. Sahihi ya mwanafunzi ……………………………Tarehe…………

Mimi mzazi/mlezi wa ……………………………………………………….ninakubali/sikubali jukumu la ulipaji wa ada na michango ya shule.

Jina la mzazi/mlezi …………………………………………………………Sahihi………………

Tarehe ……………………………………………

| Picha ya mzazi / mlezi | Picha ya mzazi / mlezi |
|---|---|

Ndugu wa karibu aliyeidhinishwa na mzazi/mlezi anayeweza kupewa taarifa au kuja kumtembelea mwanafunzi au kupewa taarifa za mwanafunzi endapo mzazi /mlezi hapatikani.

Jina kamili ...............................................................

Uhusiano wake na mwanafunzi ........................................................ namba ya simu ...................

| Picha ya ndugu wa karibu |
|---|